

IMAANI YA NGUZO ZAKE.

Imaan:

Imaani ni maneno, vitendo na Itikadi.

Imaani inazidi kwa kuyafanya matendo mema ya kumtii Allah (sw), na inapungua imaani kwa kufanya matendo mabaya ya kumuasi Allah.

Nayo ni maneno yaliyomo moyoni na kutamkwa kwa ulimi, na matendo ya moyoni, kwa kutamka kwa ulimi na kafanya kazi viungo.

Kauli ya moyoni ni kuitakidi na kusadikisha moyoni, na kauli ya ulimi ni kukiri.

Na matendo ya moyo ni kujisalimisha, kujitakasa na kutangaza, kupenda, kufanya yaliyo mema.

Kufanya kazi viungo ni kuyafanya yaliyoamrishwa na kujiepusha na yaliyo katazwa.

Kwa hakika imewekwa wazi kwenye Quran na Sunnah za bwana Mtume (saw) ya kwamba Imaan ina nguzo zake, ambazo ni;

- 1: kumuamini Allah (sw)
- 2: Kuwamini malaika wa Allah.
- 3: Kuamini Vitabu vya Allah.
- 4: Kuwaamini Mitume wa Allah.
- 5: Kuamini siku ya mwisho.
- 6: Kuamini qadar ya Allah, kheri ni shari vyote ni vya Allah.

قال تعالى: ﴿أَمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلُّ أَمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ﴾ [الفرقة: ٢٨٥].

Allah (sw) anasema: ("Ameamini mtume wa mwenyezi mungu, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa mola wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuaamini mwenyezi mungu ya kuwa ana malaika, ameteremsha vitabu na ametuma mitume, na hatukanushi yejote katika mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia msamaha wako mola wetu, na kwako pekee ndio marejeo") (Al-Baqarah :285).

Na kama ilivyokuja katika sahihi Muslim kutookana na Hadithi ya Amir Muuminina Umar bin Khatwab (R.A) ya kwamba bwana Mtume (saw) anasema:

كما جاء في صحيح مسلم من حديث عمر بن الخطاب رضي الله عنه: (أن جبريل - عليه السلام - سأله النبي - صلوات الله عليه - عن الإيمان ، فقال له : «الإيمان أن تؤمن بالله ، وملائكته ، وكتبه ، ورسوله ، واليوم الآخر ، وتؤمن بالقدر خيره وشره ») [مسلم: ٨].

("Hakika ya Jibir alayhi salaam alimuuliza mtume (saw) kuhusuana na Imaani, Mtume akamjibu akasema Imaan, ni kumuamini Allah, na Malaika wake, Kuamini vitabu vyake, kuamini Mitume wake, kuamini siku ya mwisho, na kuamini qadar kheri na shari") (Ameipokea Imamu Muslim).

Kwa haya mambo sita, ndio misingi mikuu ya Aqeeda sahihi ambayo iliteremka kwenye kitabu cha Allah (Quran), na ndiyo ambayo alitumilizwa kwayo bwana Mtume (saw) na ndio inayoitwa NGUZO ZA IMAAN.